JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA SITA

03 NOVEMBA, 2026

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

_____

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA SITA – TAREHE 03 NOVEMBA, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 na tarehe 30 Juni, 2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa

Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 na tarehe 30 Juni, 2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

76. MHESHIMIWA KASSIM HASSAN HAJI (MWANAKWEREKWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Vijana waliomaliza Vyuo kupata nafasi za *internship* ili wapate uzoefu wa kazi.

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

77. MHESHIMIWA JAPHAEL MASANJA LUFUNGIJA (ULYANKULU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Mto Igombe kwenye Barabara ya King'wangoko Usonga ili ipitike kwa kipindi chote cha Mwaka.

78. MHESHIMIWA EMMANUEL JOHN KHAMBAY (BABATI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Soko Kuu la kisasa katika Halmashauri ya Mji wa Babati litakalozingatia mahitaji ya makundi yote ya Wafanyabiashara.

79. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Wodi ya Wazazi na Jengo la Maabara Kituo cha Afya Oldeani - Karatu.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

80. MHESHIMIWA JAMILA MAHMOUD JUMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha upangaji wa Watumishi kwa kuzingatia maslahi ya kifamilia zaidi kwa wanaotoka Zanzibar.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

81. MHESHIMIWA JANETH ELIAS MAHAWANGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, kuna mpango gani maalum wa kutenga Viwanja, Majengo au maeneo ya Viwanda vidogo kwa ajili ya Wanawake Wajasiriamali wa Tanzania.

WIZARA YA FEDHA:

82. MHESHIMIWA TIMIDA MPOKI FYANDOMO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha dirisha maalum la Vijana katika Benki za Biashara nchini.

83. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini utaratibu wa kutoa taarifa Bungeni kuhusu fedha zinazopatikana kwenye Migodi mikubwa ya Madini, Mafuta na Gesi kila Mwaka utaanza.

WIZARA YA MAJI:

84. MHESHIMIWA MARIRTA GIDO KIVUNGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Maji Monduli unaotarajiwa kunufaisha Vijiji saba utakamilika ikizingatiwa Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tangu Mwaka 2024.

85. MHESHIMIWA DEVOTA MATHEW MINJA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua Bwawa la Mindu – Morogoro.

86. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji wa Sayaka – Mahaha katika Tarafa ya Ndagula yenye Vijiji 18.

WIZARA YA UJENZI:

87. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (BAGAMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Makofia – Mlandizi kwa kiwango cha lami.

88. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Rwantege Kona Kijiji cha Rutenge – Nshamba kuelekea Mushabago kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

89. MHESHIMIWA FATMA ALLY REMBO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa ajira kupitia Sekta ya TEHAMA kama *Freelancing, Coding* na ubunifu wa kidigitali kwa Vijana na Wanawake.

90. MHESHIMIWA ZULFA MMAKA OMARY (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufikisha huduma ya *Fiber* Mlangoni Mijini na Vijijini kutokana na uhitaji mkubwa uliopo kwa Wananchi.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

91. MHESHIMIWA FARAJI BURIANI NANDALA (NDANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itatatua mgogoro wa mpaka kwenye Kitongoji cha Mpanyani Kata ya Nangoo ili kijulikane kipo Masasi au Newala.

WIZARA YA NISHATI:

92. MHESHIMIWA KIJAKAZI YUNUS MOHAMED (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Mikoa ya Kusini hususani Lindi inaingia kwenye Gridi ya Taifa ya Umeme.

WIZARA YA AFYA:

93. MHESHIMIWA DKT. CATHERINE CANUTE JOACHIM (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza kiwango cha udumavu kwa Watoto chini ya miaka mitano kutoka 30% hadi 20% ifikapo 2030.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

94. MHESHIMIWA EDWARD KISAU OLELEKAITA (KITETO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za kumalizia Mradi wa Bwawa la Kaiwang Kata ya Ndedo Kiteto.

WIZARA YA KILIMO:

95. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Matrekta ya bei nafuu yataanza kuuzwa Momba ili kuondokana na jembe la mkono.

IV. HOJA ZA KAMATI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 na tarehe 30 Juni, 2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 na tarehe 30 Juni, 2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

DODOMA **BARAKA I. LEONARD**
03 NOVEMBA, 2026 **KATIBU WA BUNGE**